Mambo ambayo vijana wanapaswa kujua kuhusu

# USAFIRISHAJI HARAMU WA WATU KWA MADHUMUNI YA KINGONO NA KUTUMIWA VIBAYA

## Usafirishaji haramu wa watoto kwa madhumuni ya kingono ni nini?

Ni aina mbaya ya unyanyasaji wa watoto inayohusisha kijana aliye chini ya umri wa miaka 18 kushiriki katika tendo la kingono kwa kubadilishana na pesa au kitu chenye thamani, bila kujali kama kulikuwa na kulazimishwa, udanganyifu, au vitisho.



## Usafirishaji haramu wa watu kwa madhumuni ya kingono hutokea wapi?

Usafirishaji haramu wa watu unaweza kutokea **popote**.

Wanaofanya usafirishaji haramu wa watu wanazidi kutumia mitandao ya kijamii na Mtandao kuwarubuni vijana.
Usafirishaji haramu wa watu unaweza kutokea katika maeneo kama hoteli, biashara, au nyumba. Unaweza pia kutokea kwenye Mtandao kwa kutumia teknolojia, kama vile kupiga na kutuma picha au video za kingono mtandaoni.



Watu wazima wengi na maeneo mengi ni salama, lakini ni muhimu kukumbuka kwamba wanaofanya usafirishaji haramu wa watu kwa madhumuni ya kingono hawaonekani kila wakati kuwa hatari. Ni muhimu kutambua dalili ili uweze kujilinda na kupata msaada unapouhitaji.

## Ni nani wafanyabyashara ya ngono na wanunuzi ni akina nani?



Wanaofanya usafirishaji haramu wa watu na wanunuzi wanaweza kuwa wa jinsia yoyote, utaifa wowote, au umri wowote. Wanaweza kuwa:

- Wanaokupa kazi
- Washiriki wa familia
- Watu usiowajua
- Marafiki au wenzi
- Wapenzi


## Dalili 10 za onyo kwamba usafirishaji haramu wa watu kwa madhumuni ya kingono au kutumiwa vibaya kunaweza kuwa kunatokea



**Ikiwa mtu...**

- Anakugusa mahali ambapo hutaki kuguswa;
- Anasema unadaiwa kitu na lazima ufanye wanachotaka ili kulipa deni;
- Anakuomba ukose shule au uwe nje usiku sana katika saa zisizo za kawaida;
- Anaomba au anachukua picha au video zako bila nguo;
- Anatishia kukudhuru wewe au wapendwa wako, au anatishia kupiga simu polisi au mamlaka ya uhamiaji ikiwa hutafanya wanachosema;
- Anakupa zawadi, pesa, dawa za kulevya, chakula, au makazi kwa kubadilishana na matendo ya kingono;
- Anadhibiti mahali unapoenda na watu unaozungumza nao; anakutenga na marafiki na familia;
- Anashikilia pasipoti yako, nyaraka zako, pesa zako, au simu yako;
- Anaku omba useme uongo kuhusu umri wako;
- Anaku omba uweke siri kuhusu mambo mnayofanya pamoja au mnayopanga kufanya pamoja.

## Unawezaje kupata msaada ikiwa wewe au mtu unayemjua anaweza kuwa katika hali ya usafirishaji haramu wa watu kwa madhumuni ya kingono?



**Una haki**, na hizi ni hatua unazoweza kuchukua ikiwa haki hizo zinakiukwa.

- Zungumza na **mtu mzima wa kuaminika**.
- Piga simu **polisi** wa eneo lako au **911** katika hali ya dharura, au kuripoti mtu anayekunyanyasa au anayekutumia vibaya.
- Piga simu **Nambari ya Kitaifa ya Msaada dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Watu**. Ziko wazi saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki.

**Simu**: 1-888-373-7888

**Tuma ujumbe kunako**: 233733

**Live Chat**: https://humantraffickinghotline.org/en/chat



The production of this material was supported by Grant #90RB0054 from the Administration for Children and Families (ACF). Its contents are solely the responsibility of the U.S. Committee for Refugees and Immigrants (USCRI) and do not necessarily represent the official views of ACF.

U.S. COMMITTEE FOR REFUGEES AND IMMIGRANTS